# DARASA LA SABA - 2020

**Muda: Saa 1 Dakika 40.**

# KISWAHILI:
# SEHEMU YA KWANZA:
# LUGHA

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**
**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI.**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu, andika katika kijitabu hiki.
3. Ukiisha kuchagua jibu lako, lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU.**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba umeandika yafuatayo katika karatasi ya majibu:

**JINA LAKO**

**JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani nambari ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu, na usiikunje.
9. Kwa kila swali **1-50**, umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi **A, B, C, D**. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

**Katika kijitabu cha maswali:**

**19. Jibu kitendawili kifuatacho**

Mwanangu analia mwituni ________

A. Jino B. Firigisi C. Shoka D. Magurudumu

Jibu sahihi ni **C**

Katika karatasi ya majibu

16. [A] [B] [C] [D] 17. [A] [B] [C] [D] 18. [A] [B] [C] [D] 19. [A] [B] [C] [D]

19, kisanduku chenye herufi **C** ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja** tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kujazia nafasi zilizoachwa wazi.***

Likizo __1__ niliamua kumtembelea rafiki __2__ Fazaa. Kumbuka mimi __3__ niliyemfadhili alipojiunga na chuo kikuu. Hivyo basi niliposikia kuwa alitumwa kufanya kazi katika shirika __4__ fedha duniani, niliamua kumzuru. Hata hivyo mambo __5__ upande wangu. __6__ kunipa makaribisho ya hedhi, alimwambia __7__ aseme hakuwa. Kweli __8__.

**1.** **A.** uliopita **B.** lililopita **C.** iliyopita **D.** zilizopita

**2.** **A.** yangu **B.** wangu **C.** zangu **D.** langu

**3.** **A.** ndiye **B.** ndimi **C.** ndio **D.** ndiwe

**4.** **A.** ya **B.** za **C.** cha **D.** la

**5.** **A.** yalienda mserego **B.** yalienda mvange **C.** yaliniwia vyema **D.** yalinikulia vizuri

**6.** **A.** Baada ya **B.** Kabla ya **C.** Badala ya **D.** Zaidi ya

**7.** **A.** bawaba **B.** bawabu **C.** kuli **D.** mshenga

**8.** **A.** akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki. **B.** akumlikaye mchana usiku atakuchoma
**C.** apendwaye akajua haachi kujishaua **D.** asante ya punda ni mateke

Somo la Kiswahili __9__ kustahika. Leo hii __10__ hapo awali, Kiswahili ni lugha ya taifa na rasmi. Kwa sasa lugha hii inatumiwa __11__ Kiingereza katika nyanja mbalimbali. Ningetaka wale ambao hawajalikumbatia somo __12__ wajue kuwa watabaki __13__. Nao wazungumzaji wahakikishe kuwa wanatumia aina __14__ za maneno kama vile vihusishi. Mifano ya vihusishi ni __15__.

**9.** **A.** inazidi **B.** linazidi **C.** kinazidi **D.** unazidi

**10.** **A.** sawa na **B.** sawia na **C.** sambamba na **D.** kinyume na

**11.** **A.** sawa na **B.** sambamba na **C.** kando na **D.** kando ya

**12.** **A.** hili **B.** huu **C.** hiki **D.** huyu

**13.** **A.** nyuma mithili ya koti **B.** nyuma mithili ya tai
**C.** nyuma mithili ya kiatu **D.** nyuma mithili ya soksi

**14.** **A.** yote **B.** wote **C.** lote **D.** zote

**15.** **A.** bora, stadi, chafu, safi **B.** vizuri, vibaya, kimoyomoyo, sana
**C.** kuliko, kwenye, -ni, katika **D.** ingawa, lakini, lau, hata hivyo

***<u>Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi</u>***

**16.** **Chagua kiwakilishi katika sentensi ifuatayo:**

Hawa ni wachezaji shupavu.

A. Hawa

B. ni

C. wachezaji

D. shupavu

**17.** **Tambua matumizi ya -wa-**

Uzi mweupe <u>wa</u> kushonea umenunuliwa.

A. Kuonyesha kumiliki.

B. Kuonyesha matumizi.

C. Kuonyesha kitenzi.

D. Kuonyesha hali.

**18.** Gani si kiungo cha kupikia?

A. Bizari

B. Karafuu

C. Dania

D. Mpunga

**19.** **Andika sentensi ifuatayo bila kutumia -amba-:**

Uyoga ambao ulinunuliwa ni wangu.

A. Uyoga ulionunuliwao ni wangu.

B. Uyoga ulizonunuliwa ni wangu.

C. Uyoga uliyonunuliwa ni wangu.

D. Uyoga ulionunuliwa ni wangu.

**20.** **Chagua wingi wa sentensi ifuatayo:**

Jani hilo kavu lilipeperushwa likatua kwenye mlingoti.

A. Majani hayo makavu yalipeperushwa yakatua kwenye mlingoti.

B. Majani yale makavu yalipeperushwa yakatua kwenye milingoti.

C. Majani yale makavu yalipeperushwa yakatua kwenye mlingoti.

D. Majani hayo makavu yalipeperushwa yakatua kwenye milingoti.

**21.** **Maneno yaliyopigiwa kistari katika sentensi ifuatayo ni:**

Mzazi <u>wangu</u> amefika lakini <u>wako</u> atafika kesho.

A. Kielezi, kiwakilishi

B. Kivimishi, kiwakilishi

C. Kiwakilishi, kivumishi

D. Kivimishi, kielezi

**22.** Ni sentensi gani imetumia -kwa- ya kuonyesha jinsi ya kufanya jambo?

A. Mchinjaji alikata nyama kwa kisu.

B. Mwalimu alinipa alama nane kwa kumi.

C. Mwanafunzi amemwamkua mwalimu wake kwa heshima.

D. Mkimbizi alituzwa kwa kushinda mbio hizo.

**23.** **Tambua matumizi ya 'ka'**

Kampelekee pesa zako zote!

A. Kusudi

B. Amri

C. Kuonyesha mshangao

D. Kutoa wito

**24.** **Udogo wa sentensi ifuatayo utakuwa gani?**

Ndovu na ndama wameangusha miti njiani.

A. Dovu na dama yameangusha majiti jiani.

B. Kidovu na kidama kimeangusha miti njiani.

C. Kidovu na kidama vimeangusha vijiti vijiani

D. Madovu na madama yameangusha majiti majiani.

**25.** Ni sentensi gani iliyo katika kauli ya kutendesha?

A. Alimwogofya mzazi ili asiadhibiwe kijeshi

B. Mtoto akililia wembe mpe.

C. Somo lilielewaka vizuri mara hii.

D. Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki.

**26.** **Andika kwa tarakimu:**

100,000

A. Milioni moja

B. Elfu kumi

C. Laki moja

D. Laki mia moja

**27.** Kula - kura, fuma - vuma, chambo - jambo ni mifano ya

A. visawe

B. vitate

C. vitawe

D. vibadala

**28.** -angu, -etu, -ako, -enu ni vimikilishi. Mimi, sisi, nyinyi, yeye ni

A. nafsi

B. viambishi

C. virejeshi

D. vielezi

**29.** **Kanusha:**

Utaenda kulima kisha mtasoma.

A. Utaenda kulima kisha hamtasoma.

B. Hutaenda kulima wala hamtasoma.

C. Hamtaenda kulima na hamtasoma.

D. Sitaenda kulima wala hatutasoma.

**30.** Nomino 'ndizi' iko katika ngeli gani?

A. I - ZI

B. LI - YA

C. I - I

D. U - I

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.***

Ajali nyingi zinazidi kushuhudiwa humu nchini mwetu. Hata kama wahenga husema kuwa ajali haina kinga,mimi siwezi kukubaliana na kauli hiyo kabisa. Tuko na sababu tele zinazosababisha ajali. Hata hivyo sababu kuu kabisa ni utepetevu wa binadamu. Ajali yoyote inayohusika lazima pawe na mahali ambapo binadamu alikosa kutekeleza wajibu wake ipasavyo. Hii basi inamaanisha kuwa, kama binadamu atajikosoa, ajali karibu zote zinaweza <u>kudhibitiwa.</u>

Juzi ama ni jana? Haidhuru! Cha muhimu ni kuwa nilisikitika sana kuona watu sita wa familia moja wakiangamia katika ajali moja. Iwapo ungechunguza kwa macho ya kionambali ungeona kuwa ajali kama hiyo ingeepukika. Jambo jingine la kuvunja moyo ni kuona wenye mabaa wakifunga safari kuelekea mahakamani kupinga matumizi ya kidude cha kutambua iwapo dereva amepitisha kiwango cha ulevi. Mahakama ya rufaa tayari imetoa uamuzi wake ambao unapinga matumizi ya kidude hiki. Ati ni kinyume cha sheria. Swali ni je, maisha na sheria ni kipi cha muhimu? <u>Jibu lake unalijua fika.</u> Hebu jiulize, kwa nini madereva wengi wamefurahia uamuzi huo? Majaji ni wazuri lakini uamuzi mwingine wao, ni wa kutiliwa shaka.

Tumeona na hata kusikia viongozi mashuhuri wakihusika katika ajali. Miongoni mwa sababu zinazoleta maafa ni uendeshaji wa kasi kupita kiasi. Tumeshuhudia madereva wengi wakin'goa vidhibitimwendo na pia hawairekebishi mikanda ya usalama. Aidha magari yao hayakaguliwi. Kinachoyafanya magari haya kuonekana barabara ni uzito wa wenye magari na njaa ya maafisa wa trafiki. Askari akipigwa konde la nyuma, analikubalia gari bovu kupita. Hatima yake?

Ulevi pia huchangia ajali. Dawa za kulevya mathalani mirungi na bangi hutumiwa sana na madereva hawa. Matokeo yake huwa ni ajali mbaya sana. Hata kama ninawalaumu majaji wetu, serikali nayo lazima izikarabati barabara zetu ambazo ziko katika hali ya kutamausha. Ziwe za lami zimejaa mashimo ungedhani ni makongo ya kupanda miche ya ndizi. Zile zisizo za lami zimeharibika kiasi kwamba ni vigumu kuzitofautisha na mapito ya mifugo. Usije ukajidanganya kuwa serikali haikutenga pesa za ktuosha. Huo ni uongo pesa ziliachwa na kutengwa lakini zilifaidi wachache wasiogusika.

Abiria nao waelimishwe kuhusu ajali. Abiria waonyeshwe hatari ya kuabiri gari lililojaa abiria. Wajue kuwa ni jukumu lao kuwaarifu maafisa wa usalama endapo dereva anaendesha gari kwa kasi ile isiyokubalika.

Kuna tetesi kuwa polisi ndio kizingiti kikubwa sana kinachokwamiza juhudi za kukabiliana na ajali. Hii ni kwa sababu wamekuwa wakirambishwa asali iliyo tamu kwao lakini chungu kwa raia.

Hebu nimalizie kwa kusema kuwa, njia ya pekee ya kukomesha ajali ni kukomesha yote mabaya na kuhakikisha yote muhimu yanafuatwa bila kushurutishwa.

**31.** Mwandishi anaonekana,

A. angetoa methali nzuri kuliko ile iliyotolewa na wahenga.

B. kukataa kuwa wahenga ndio watu wa pekee wanaojua methali.

C. kupinga kauli ya wahenga.

D. kudai kuwa ajali zote zinazotokea huwa hazileti maafa yoyote.

**32.** Chanzo kikuu cha ajali kulingana na aya ya kwanza ni

A. barabara mbovu.

B. alama za barabarani zisizosomeka.

C. mwendo wa kasi.

D. makosa ya kibinadamu.

**33.** Unadhani ni kwa nini wenye mabaa walielekea mahakamani?

A. Walinuia kupewa kibali cha kuuza pombe hata wakati usiofaa.

B. Walitaka kuhakikisha afya yao na watoto wao iko imara.

C. Kidude cha kukagua unywaji wa pombe kupita kiasi kilikauka kanuni za afya.

D. Walihofia kuwa kidude cha kukagua unywaji wa pombe kingedidimiza biashara zao.

**34.** <u>Kudhibiti</u> kulingana na kifungu ni

A. kumalizika B. kupungua

C. kuzuilika D. kusahaulika

**35.** Gani haisababishi ajali?

A. Kung'oa vidhibiti mwendo.

B. Kuendesha magari kwa kasi.

C. Kuendesha magari mabovu.

D. Kuendesha magari kwa kasi kupita kiasi.



GEUZA UKURASA

36. Kupigwa konde la nyuma ina maana ya

A. kuchapwa
B. kuhongwa
C. kutukanwa
D. kudhulumiwa

37. Matokeo ya dawa za kulevya kwa abiria ni

A. kufika salama salimini.
B. magonjwa ya moyo.
C. ajali mbaya.
D. uchafuzi wa mazingira.

38. Wananchi wana jukumu gani katika kuzuia ajali za barabarani?

A. Kuwaarifu wenye magari kuhusu madereva wabaya.
B. Kuboresha barabara mbovu.
C. Kuchukua sheria mikononi mwao.
D. Kuyaambaa magari yaliyojaa abiria.

39. Jibu lake unalijia fika. Yaani

A. sheria ni muhimu kuliko maisha.
B. maisha ni muhimu kuliko kidude.
C. kidude ni muhimu kuliko maisha.
D. maisha ni muhimu kuliko sheria.

40. Njia bora zaidi ya kuzuia ajali ni

A. kuhakikisha maafisa wa polisi hawahongwi hata kidogo.
B. kutengenezewa barabara nyingi zilizosakifiwa.
C. kurekebisha chochote kibaya katika sekta ya uchukuzi.
D. kununua magari mapya yenye mikanda ya usalama.

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.</u>***

Hapo zamani za kale paliishi mfalme mmoja mwadilifu aliyekuwa na paka, ng'ombe, mbuzi na kondoo katika boma lake. Mifugo wote waliishi ndani ya boma na paka naye aliishi kwa kuwinda panya waliokuwa katika ghala kubwa ya nafaka.

Basi wakati mmoja ulitokea mkasa uliomfanya paka kukosa mawindo yake kwa zaidi ya siku tano. Kijana mmoja mtundu alitega mtego wa panya kwenye tundu la kuingilia katika ghala ya nafaka. Kwa kawaida aila ya mfalme haikuwa na mazoea ya kumpa chakula paka kwa kujua alikuwa akitegemea mwenyewe kwa kuwinda. Ijapokuwa paka alilia sana kwa shida ya njaa, hakutiliwa maanani. Paka alianza kudhoofika kwa ukosefu wa chakula. Alipokwenda tena kuangalia njia aliyokuwa akiingilia ghalani, mtego ulikuwa papo hapo na kama angejaribu kujiingiza mtego ungemnasa. <u>Alikata shauri</u> kuwafuata ng'ombe, mbuzi na kondoo kutafuta msaada wao. Alikuwa na yakini kuwa mmoja wao angeweza kuusukuma mtego kwa pembe na kuufyatua bila ya kudhurika. Wenzake, lakini walimpuuza na hata kumjibu kwa kejeli.

"Sikiliza paka. Sisi ni walaji nyasi na tuna shauri moja tu la kukupa. Kwa nini hujifunzi kula nyasi? Hebu angalia zinapatikana kila mahali tena kwa wingi huku kwa mfalme. Nyasi hizi tumekula kuanzia mwaka jana na bado hata hazijafika nusu. Anza kuzivamia kuanzia mwisho huo."

Baada ya jibu hilo la dharau, paka hakutafuta msaada kwa yeyote. Alibaki kuchakurachakura pipa la taka kutafuta vipande vya mikate na ukoko wa ugali. Waswahili husema lisilo budi hubidi na likibidi hutendwa.

Siku ya nne, palizuka balaa na belua pale bomani pa mfalme. Ule mtego ulimkamata bafe. Binti yake mfalme alipopita karibu na lile tundu aliumwa na yule nyoka. Sumu ilienea mwilini haraka. akaanguka akafa kabla ya mganga kufika kumtopoa. Mji mzima uliingiwa na simanzi. Mfalme alikuwa akimpenda sana bintiye aliyekuwa ndiye kitindamimba wake. Watu wote wa pale mjini walihudhuria mazishi yake binti mfalme. Kwa kuwa mfalme alikuwa mashuhuri, ilimbidi atayarishe karamu kubwa ya wageni waliofika mazishini. Aliamuru yule ng'ombe, mbuzi na kondoo wachinjwe ili kukimirisha wageni.

Wakati wa alasiri, paka aliwatembelea wenzake watatu pale walipofungwa. Aliwaangalia kwa masikitiko kisha akawaambia, "mwaona sasa shida ya mtu mmoja huweza kuwasibu wengine? Mfalme ametoa amri mitego yote iondoshwe mara moja. Sasa ninaweza kuingia na kutoka ghalani ninavyo taka. Hapa nilipo nimeshiba kabisa. Sasa naamini kuwa mngejua mtaishia kuchinjwa mngenisaidia. Lakini muda huo haupo tena. Kitu ambacho sitafanya, ni kula nyama yenu. Licha ya kuwa hamkunisaidia, sitaki kuonekana kama nafurahia hali yenu."

Usiku ulipoingia,kuliandaliwa karamu ya kukata na shoka. Watu wote walikula shibe yao.

**41.** Kazi ya paka ilikuwa

A. kulinda ghala ya nafaka dhidi ya wezi wa usiku.

B.kuwinda panya waliokuwa wakiharibu nafaka za mfalme.

C. kuwakalisha mbuzi, ngombe na kondoo wakila nyasi.

D. kuwatumbuiza wageni ambao wangeingia kuhudhuria mazishi ya binti yake mfalme.

**42.** Kwa maoni yako, mtoto mtundu akiweka mtego njiani alikuwa na nia gani?

A. Alitaka kumnasa bafe aliyekuwa amewahangaisha kwa miaka mingi.

B. Alitaka kumnasa paka kwa kuwa paka alikuwa mkali sana.

C. Alidhaminia kumnasa panya aliyezoea kuharibu nafaka.

D. Alitaka kumkinga na kumzuia paka asiingie ghalani.

**43.** Ni nini hasa kilichosababisha maafa pale bomani pa mfalme?

A. Paka kukosa chakula.

B. Mtoto mtundu.

C. Kifo cha bintiye mfalme.

D. Mtego wa panya.

**44.** Ni tangazo gani la mfalme lililofurahiwa na paka?

A. Watu wengi kuhudhuria mazishi ya bintiye.

B. Kuondoshwa kwa mitego ya kila aina mijini.

C. Kuondoshwa kwa mitego ya paka.

D. Kupata kibali cha kutembea kila mahali alipotaka.

**45.** Paka alinyimwa chakula kwa kuwa

A. alikuwa na maringo mengi sana na hangekula chakula ovyo ovyo.

B. chakula chake kilikuwa tofauti na kile cha wale wengine.

C. alikuwa akipenda kujipikia chakula chake yeye mwenyewe.

D. alikuwa akijitegemea kwa kuwawinda panya.

**46.** Mwaona sasa shida ya mtu mmoja huweza kuwasibu wengine. Ni methali gani inayolenga kauli hii?

A. Mtego wa panya huingia waliomo na wasiokuwemo.

B. Mkono mmoja hauchinji ng'ombe.

C. Meno ya mbwa hayaumani.

D. Usione kwenda mbele kurudi nyuma si kazi.

**47.** Alikata shauri ina maana ya

A. kuwatetesha

B. aliamua

C. alisingizia

D. alilaumu

**48.** Ustaarabu wa paka unaonekana pale

A. anapowatembelea wenzake licha ya kuwa walisusia kumsaidia.

B. aliwaomba ng'ombe, mbuzi na kondoo kumsaidia.

C. mtoto wa mfalme anapoumwa na bafe.

D. anaonekana kufurahia madhila yaliyowafika wenzake watatu.

**49.** Baada ya paka kupata jibu la dharau,

A. aliamua kwanza kula nyasi kama wenzake.

B. aliamua kuwapiga buti marafiki zake wote.

C. aliamua kutotafuta msaada tena.

D. aliamua kujitia kitanzi.

**50.** Mfalme na bintiye walikuwa wakiishi katika

A. ikulu

B. sebule

C. kasri

D. pambizoni